# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## SHULE YA SEKONDARI TUMAINI


S.L.P.533,
**IRAMBA-SINGIDA.**
TAREHE, 29/10/2025

Mkuu wa shule*: **SEVERINA F. CHUWA***
**Simu*: 0769184185/0657971377***
***Makamu mkuu wa shule***
***0714951475/0755002094***
Barua pepe;***tumainisecondary1969@gmail.com***
**Instagram: tumainisecondaryschool**
**Facebook: Tumaini Secondary**


MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI…………………………WA S.L.P…………….

**YAH:** MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO KWA KWANZA,SHULE YA SEKONDARI **TUMAINI** HALMASHAURI YA WILAYA YA **IRAMBA** MKOA WA **SINGIDA**.MWAKA **2025**.

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) katika shule ya sekondari T**umaini** iliyoko Wilaya ya **IRAMBA** katika mkoa wa **SINGIDA** mwaka **2025; HONGERA NA KARIBU SANA TUMAINI SHULE YA SEKONDARI!**

Shule iko kilomita 70 kutoka Singida mjini.
Kama utapanda basi la moja kwa moja toka Dar es salaam, Moshi, Arusha N.K yaani mabasi yote yenye uelekeo wa kwenda Mwanza, shinyanga (barabara ya kati) utashuka kituo kinachoitwa **KITUSHA**, na hapo utapanda bodaboda au gari ndogo aina ya HIACE, ni umbali wa kilomita 8 mpaka shuleni.
Kutoka Singinda mjini utapanda mabasi katika kituo cha mabasi msufini au Jengo la CCM, hapo utakuta magari aina ya **HIACE** ambayo huondoka Singida kati ya saa 6:30 na saa 7:30 mchana kila siku kwenda Kinampanda mahali shule ilipo. Nauli kwa sasa ni shilingi **5,000**/= kama

hapatakuwa na mabadiliko, endapo utachelewa muda huo upande gari yoyote inayoenda kiomboi au Igunga katika vituo hivyo vya magari na ashuke kituo cha magari KITUSHA.

Endapo mwanao atapanda mabasi ya kutoka Tabora, Nzega, Kahama, au Mwanza kwenda Arusha au Dar es salaam ashukie sehemu iitwayo **KITUSHA**. Kilomita chache kutoka Misigiri.
Kutoka Kitusha kuna umbali wa kilomita nane (8) mpaka shuleni hivyo atakodisha pikipiki mpaka shuleni au atasubiri maabasi aina ya HIACE yatokayo Singida Mjini kufika shuleni.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **06/01/2025** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **siku ya Jumamosi 05/01/2025 muda wa kuripoti ni mchana kuanzia saa saba kamili mchana hadi saa kumi na moja na nusu jioni,** Masomo yanaanza 06**/01/2025**.

Tunasisitiza mwanafunzi awahi shule kwa muda na tarehe iliyosemwa hapo juu ili kuepusha usumbufu usio wa lazima ili kuendana na kalenda ya masomo. Kama hujaelewa kitu, ama dharura yeyote piga simu kwa namba zilizowekwa hapo juu.

## 2. MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare ya shule

a) Sare ya shule ni sketi mbili(2) ya damu ya mzee kitambaa kizito cha suti grade Namba 1 mshono wa marinda ya kufuatana, sketi iwe ndefu mpaka chini (juu kidogo ya viatu) Mashati mawili(2) meupe ya mikono mifupi.
b) Sketi mbili za kuvaa nje ya darasa rangi ya Ugoro mshono (marinda ya kufuatana. sketi iwe ndefu mpaka chini (**juu kidogo ya viatu**).
c) Wanafunzi wanaovaa hijabu (kijuba) iwe nyeupe na ndefu kufika usawa wa nyonga, na hijabu zote ziwe za kitambaa cheupe aina ya **halua** au **babi.** (sio kitambaa cha mpira au aina nyingine)
d) Pull neck (kabashingo) nyeupe
e) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi-Jozi mbili(2)
f) Sare za michezo kwa shule hii ni bukta na T-shirt rangi ya bluu, raba rangi yoyote (jozi moja) na track suit rangi ya blue bahari (jozi moja)
g) Soksi nyeupe jozi tatu.
h) Sweta rangi ya ugoro.[kwa mzazi anayehitaji kununulia shuleni linapatikana lenye nembo ya shule kwa tsh. 15,000/= tu)
i) T-shirt mbili (2) zenye nembo ya shule za kuvaa nje ya darasa kwa mzazi anayehitaji kununulia shule zinapatikana kwa shilingi 30,000/=
j) Nembo ya shule kwa ajili ya mashati inapatikana shuleni kwa shilingi 5,000 tu kwa kila shati.
k) Nguo za nyumbani haziruhusiwi isipokuwa aje na kanga/vitenge pair moja tu atatumia wakati wa kuoga.

**NB:** KAMA UTAPATA MKANGANYIKO WA RANGI YA SKETI [DAMU YA MZEE AU UGORO] UNARUHUSIWA KUJA KUSHONEA HUKU, JIRANI NA SHULE KUNA MAFUNDI

**2.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

**2.3.1.Vifaa vya darasani**

(a) Madaftari makubwa 11 (counter book quire 3 na 4) madaftari ya mazoezi madogo aina ya msomi (11) (b) Kalamu za wino (c) Mathematical set

(d) Ream A4 moja ya karatasi kwa ajili ya mitihani
(e) Penseli
(f) Rula
(g) Dictionary
(h) Aje na faili 1 (i) Aje na vitabu kulingana na masomo yake kwa ajili ya kujifunzia

**2.3.2. Vifaa vya kulalia**

(a) Godoro (sponji) futi 2.5 inch 4 (b) Net ya Mbu nyeupe ya duara
(c) Mashuka mawili(2) light blue (e) Mto wenye foronya light blue (f) Blanketi 1

**2.3.3. Vifaa vya chakula**

(a) Sahani (b) Bakuli (c) kijiko (d) kikombe (e) Galoni ya kuwekea maji ya kunywa

**2.3.4. Vifaa vya usafi binafsi**

(a) Ndoo 2 (lita 20 na lita 10) (b) Mswaki na dawa ya meno (c) Malapa (d) Sabuni za kufulia na kuogea.

Mahitaji ya kike (nguo za ndani za kutosha na taulo za kike za kutosha hata kama mtoto hajavunja ungo), (e) Mkasi wa kunyolea nywele, wanafunzi wote wana nywele fupi.

**VIFAA VYA USAFI**

a)Ufagio wa chelewa, b) Jembe lenye mpini, ufagio mgumu wa brashi (hard broom) 1, dawa ya chooni aina ya ARO.

**ANGALIZO: KUHUSU AFYA**

**WANAFUNZI WAJE NA BIMA YA AFYA!** KAMA HANA BIMA YA AFYA AJE NA PESA TASLIM SHILINGI shilingi 6,000/= kwa ajili ya kukatiwa bima ndogo ( CHF)

NINAWATAKIA MAANDALIZI MEMA, KARIBU SANA TUMAINI SEKONDARI, KWETU SISI "**ELIMU NI USHINDI**"

____________________

SEVERINA F. CHUWA
**MKUU WA SHULE**

# SHULE YA SEKONDARI TUMAINI.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

i. **Utoro**
ii. **Wizi**
iii. **Uasherati, ushoga na ulawiti , Kuoa au kuolewa.**
iv. **kutoa mimba.**
v. **Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya .**
vi. **Uvutaji wa sigara au bangi.**
vii. **Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.**
viii. **Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.**
ix. **Kudharau Bendera ya Taifa**
x. **Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule**
xi. **Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni**
xii. **Kugoma kwa namna yoyote au kuchochea vurugu**
xiii. **Kutoa lugha ya matusi au lugha chafu kwa mwanafunzi,walimu,walezi,na jamii kwa ujumla.**
xiv. **Kumdharau mwalimu, Kiongozi, Mfanyakazi na jamii kwa ujumla**
xv. **Kutohudhuria vipindi kwa uzembe**
xvi. **Kutofanya mitihani kwa makusudi/bila sababu ya msingi**
xvii. **Kushirki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.**
xviii. **Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k**
xix. **Kumiliki simu.**

**FOMU A:**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

| |
|---|
| Picha<br><br>Ya<br><br>mwanafunzi |

**SHULE YA SEKONDARI TUMAINI.**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA MWANAFUNZI**

A. **Habari za mwanafunzi**:

i. Jina kamili……………………………………………………………….

ii. Tarehe ya kuzaliwa………………………..Wilaya……………………………

iii. Dini………………………Dhehebu……………………………………….

**Mahali atakapokuwa anaenda likizoni:**

i. Jina…………………………Uhusianao……………..Mahali……………..

ii. Jina…………………………Uhusiano………………Mahali……………..

**Kukubali nafasi:**

Mimi……………………………………nimeona maelekezo ya kujiunga na shule ya Sekondari Tumaini. Nakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na kutii sheria za shule. Nitakapokuwa shuleni, nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kusoma kwa bidii na kuchapa kazi za mikono kwa bidi, kutunza mazingira, kushiriki kikamilifu ratiba yote ya shule ili kutimiza lengo la kupata elimu katika ujumla wake NA NINAAHIDI KUWA MWANAFUNZI MWEMA, MTIIFU MWENYE NIDHAMU YA HALI YA JUU NIKIONGOZWA NA MOTTO WA SHULE "**ELIMU NI USHINDI**"

**Saini……………………..Tarehe……………………………………………………….**

B. **Habari za Mzazi/Mlezi**

| |
|---|
| Picha<br><br>Ya<br><br>Mzazi/mlezi |

i. Jina kamili……………………………………………………………

ii. Yeye ni mzazi au mlezi………………………………………………

iii. Uhusiano uliopo na mwanafunzi……………………………………….

iv. Kazi yake……………………………………………………………

v. Anwani ya kazini……………………………………………………

vi. Namba ya simu……………………………………………………….

vii. Anwani ya nyumbani…………………………………………………………

viii. Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi:

Nimehakikisha maelekezo na maagizo yameeleweka na mtoto wnagu atafuata sheria na taratibu zote za shule ya sekondari Tumaini.

**Jina…**…………………………………..**Saini……………………Tarehe**………………

FORM B:

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

PART A:

**TO**: The Medical Officer
_________________________
_________________________
_________________________

FROM: The Headmistress
Tumaini Secondary School
P.O.BOX 533 Kinampanda
IRAMA-SINGIDA

NAME OF THE STUDENT___________________________________

Please examine the above named Student as to her fitness for joining our Secondary School 2024

Signature ___________________________

PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by Medical Officer)

I have examined the above named person and discovered that she is____________
_____________________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________________

Date________________________ Signature ____________________________
Station_____________________ Designation _________________________